

SEHEMU YA 1: Taarifa za Mkopaji, Ombi la Mkopo, na Hati za Kuthibitisha

JINA		
ANWANI		
JIMI	JIMBO	MSIMBO
NAMBARI YA SIMU:	BARUA PEPE	

Maelezo mafupi ya ombi la mkopo na jinsi mkopo utatumika.	Orodha ya ukaguzi wa hati za kuthibitisha kujumuishwa na maombi. ☐ Mpango wa biashara ya shamba (ukurasa wa 1 hadi 2). ☐ Mpango wa biashara unajumuisha mpango wa uuzaji/mikataba. Taarifa ya hali ya kifedha ☐ (ikiwemo ya shamba na ya kibinafsi). ☐ Mapato halisi ya kina na ratiba ya malipo ya mkopo.
---	---

SEHEMU YA 2: Vigezo vya Kustahiki na Uthibitisho wa Mwombaji

Tia alama kwa ndiyo (Y) au la (N) kuhusiana na kila mojawapo ya kauli zifuatazo. Wakati watu wawili au zaidi wametuma maombi kwa pamoja, neno "Mimi" litamaanisha "sisi", lakini ni mtu mmoja tu anayehitaji kutimiza vigezo vya 2, 3, 5, na 6.

KIGEZO CHA KUSTAHIKI		NDIYO	LA
1	Mimi ni mkazi halali wa Jimbo la Minnesota.	☐	☐
2	Mimi ni mwanachama wa kikundi kinacholindwa (Sheria ya Mn 43A.02, Sub 33) au asiye raia lakini ninastahiki (Sheria ya MN) 256B.06, sub 4, par (b)).	☐	☐
3	Mimi ndiye mwendeshaji mkuu wa shamba linalofadhiliwa, ninakuza mazao maalum au mifugo inayostahiki.	☐	☐
4	Nina hitaji la kifedha na uwezo wa kurejesha mkopo huo.	☐	☐
5	Ninakubali kufanya kazi na mkopesaji wa kati au mtu binafsi/shirika linaloshiriki ili kukuza ujuzi na uwezo wa uzalishaji na usimamizi wa shamba langu katika muda wote wa mkopo huu.	☐	☐
6	Nina mpango wa uuzaji na/au kandarasi ya kuuza mazao au mifugo ninayozalisha (angalia mpango wa biashara wa shamba ulioambatanishwa).	☐	☐

Baadhi ya taarifa unazoombwa utoe kama sehemu ya ombi lako la mkopo zimeainishwa kama data ya kibinafsi chini ya Sheria ya Minnesota Sura ya 41B.211. Taarifa utakazotoa zitatumika tu kubainisha sifa zako za kupata mkopo. Hutakiwi na sheria utoe taarifa zilizoombwa; hata hivyo, ukichagua kutotoa taarifa zote zilizoombwa katika ombi, maombi yako yatakuwa hayajakamilika na huenda yasiweze kuchakatwa. Data ya faragha uliyotoa inaweza kutumwa kwako tu na kwa mashirika ya serikali ambayo yameidhinishwa na sheria kuipata. Mashirika ambayo yanguweza kufikia data yako ya kibinafsi yanajumuisha, lakini hayajakomea kwa, Mamlaka ya Fedha Vijijini ya Minnesota, Idara ya Kilimo ya Minnesota, Idara ya Usimamizi na Bajeti ya Minnesota, na Mkaguzi wa Sheria.

SAHIHI	MUME/MKE	TAREHE
--------	----------	--------

SEHEMU YA 3: Maelezo ya Mkopeshaji wa Kati

JINA LA MKOPESHAJI WA KATI		MTU WA KUWASILIANA NAYE	
Nambari ya Mkataba			
ANWANI		S.L. P.	
JIJI		JIMBO	MSIMBO
NAMBARI YA SIMU:		NAMBARI YA FAKSI	
FED. NAMBARI YA KITAMBULISHO		NAMBARI YA KITAMBULISHO CHA JIMBO	

SEHEMU YA 4: Masharti ya Mkopo

NAMBARI YA UTAMBULISHO WA MKOPO		
KIASI CHA MTAJI (sio zaidi ya \$20,000 au asilimia 70 ya thamani ya bidhaa za shambani, kiasi chochote kilicho chini)	\$	MATOLEO MAALUM (IKIWA INATUMIKA)
KIWANGO CHA RIBA (wasiliana na RFA kuhusiana na viwango vya juu viliopo sasa vinavyoruhusiwa)	%	
MIAKA YA KUFANYA MALIPO (sio zaidi ya miaka 6)		
MALIPO KWA MWAKA		
KIASI CHA MALIPO	\$	
TAREHE YA KUKAMILISHA		
GHARAMA ZA KUHITIMISHA	\$	

SEHEMU YA 5: Uthibitishaji wa Mkopeshaji

NINATHIBITISHA kuwa nimepitia vigezo vilivyo hapa juu pamoja na mwombaji na ninaamini kuwa mwombaji anafuata sheria za Mpango wa Majaribio ya Mikopo Midogo ya Kilimo na Makubaliano ya Mkopeshaji ambazo tumetekeleza.

SAHIHI ILIYOIDHINISHWA	CHEO	TAREHE
------------------------	------	--------

SEHEMU YA 6: Idhini ya RFA/Kukataliwa kwa Maombi

☐ IMEIDHINISHWA KWA AJILI YA MPANGO WA MAJARIBIO YA MIKOPO MIDOGO YA KILIMO NA KUHITIMISHWA KWAKE ☐ HAKUJAIDHINISHWA		MKOPO HUU UMEKABIDHIWA YAFUATAYO NAMBARI:
MAONI:		
SAHIHI ILIYOIDHINISHWA	CHEO	TAREHE

SEHEMU YA 7: Uthibitishaji wa Mkopeshaji na Kuhitimisha Mkopo

MKOPO HUU ULIHITIMISHWA TAREHE:		
SAHIHI ILIYOIDHINISHWA	CHEO	TAREHE

Maagizo ya Kutuma Maombi kwa Waombaji

Taarifa ifuatayo imeundwa ili kukusaidia katika kutuma ombi lako la Mkopo Mdogo wa Kilimo wa Majaribio kupitia Mamlaka ya Fedha Vijijini (RFA). Kabla ya kutuma maombi, utahitaji kuunda uhusiano wa kufanya kazi na kopeseshaji wa kati anayeshiriki. Ushiriki wa mkopeseshaji wa kati katika Mpango wa Majaribio ya Mikopo Midogo ya Kilimo ni wa hiari kabisa na utatofautiana baada ya muda na katika jimbo lote. RFA haiwezi kutoa mikopo ya moja kwa moja kwa watu binafsi. RFA haiwezi kushiriki katika makubaliano ya mikataba kati ya watu binafsi. RFA inaweza tu kununua mtaji wa mikopo kwa mikopo midogo ya kilimo iliyostahiki ambayo inatolewa na taasisi ya kati inayoshiriki. Kwa kushiriki katika mpango huu, RFA inaweza kuboresha kupata mkopo na kupunguza kiwango cha riba kinacholipwa na mwombaji.

Ikiwa wakati wowote, nafasi inayopatikana kwenye ombi hili haitoshi kujumuisha taarifa kwa njia halali, tafadhali jihisi huru kujumuisha ukurasa wa nyongeza. Tambulisha kila ingizo kama “angalia kiambatisho ____ ” pamoja na barua ya mwakilishi ili kuteua taarifa (mf.- angalia kiambatisho A, angalia kiambatisho B,...)

SEHEMU YA 1

Ingiza jina la mkopaji au biashara na anwani halisi. Tafadhali jumuisha nambari ya kisanduku ikiwezekana. Unaweza kuingiza majina mengi, hata hivyo, ni mtu binafsi tu aliyeorodheshwa kwanza ndiye atakayerekodiwa na RFA kama mpokeaji wa mkopo.

Katika sehemu ya taarifa za mkopo, tambulisha kiasi cha mtaji kinachoombwa na jinsi pesa hizo zinavyopaswa kutumika. Pembejeo za kila mwaka kama vile mbegu, malisho, mbolea; zinaweza kuorodheshwa kama mtaji unaofanya kazi. Fedha zinazotumiwa kwa mashine, vifaa, na rasilimali sawia zinapaswa kuorodheshwa vitofauti. Hakuna fedha zinazoweza kutumika kulipa madeni ya sasa.

Ili kusaidia katika uchakataji na uthibitishaji wa ombi hili la mkopo, hati za kuthibitisha zitahitajika. Jumuisha mpango wa biashara ya shamba uliorahisishwa, taarifa ya sasa ya hali ya kifedha (ikijumuisha maelezo ya shamba na ya kibinafsi), mapato halisi ya kina ya shughuli ya shamba, na mpango wa uuzaji katika ombi hili. Iwapo unahitaji usaidizi kutayarisha hati kama hizo, tafadhali wasiliana na Shirika la Msaada wa Mkulima wa Minnesota (MFAN) kupitia 1-877-898-6326 au www.mda.state.mn.us/mfan.

SEHEMU YA 2

Soma kwa makini kila kauli na uweke mviringo kwa “Y” ndiyo au “N” la kwa kila kauli. Ni lazima utie alama kwa ndiyo katika kila taarifa ili ustahiki kushiriki katika mpango huu. Iwapo waombaji wawili au zaidi wanatuma maombi kwa pamoja, ni mwombaji wa msingi pekee (mtu wa kwanza aliyeorodheshwa kwenye ombi) atahitaji kutimiza vipengee vya 2, 3, 5 na 6.

SEHEMU YA 3

(Sehemu hii hujazwa na mkopeseshaji wa kati.)

SEHEMU YA 4

(Sehemu hii hujazwa na mkopeseshaji wa kati.) Tambua sheria na masharti ya malipo ya mkopo. Iwapo malipo yatakuwa kwa njia inayoweza kubadilishwa au isiyo sawa, tafadhali dokeza chini ya masharti maalum (mf. - Malipo moja kwa mwezi kuanzia Julai, kabla ya tarehe 15 ya mwezi huo, kima cha chini cha \$100, malipo kamili kabla ya tarehe 15 Novemba). Jumuisha muhtasari wa gharama za kuhitimisha; ikijumuisha ada za kuwasilisha, ada za kuchataka, na gharama nyinginezo zinazohusiana na muamala wa mkopo.

SEHEMU YA 5

(Kujazwa na mkopeseshaji wa kati) Uthibitishaji wa maombi ya mkopo yaliyoidhinishwa na mkopeseshaji wa kati.

SEHEMU YA 6

(Kujazwa na RFA.) Baada ya kukamilisha sehemu ya 1 hadi 4, tuma ombi lililotiwa sahihi na maelezo ya ziada kwa ofisi ya RFA kwa ajili ya ukaguzi wa mwisho na uidhinishaji. Maombi yaliyoidhinishwa yatumwa kwa mkopeseshaji wa kati kwa ajili ya uhitimisho wa mwisho. Baada ya kuhitimishwa, makubaliano haya yatatekelezwa kikamilifu na pesa zitawekwa kwa mkopeseshaji wa kati.

SEHEMU YA 7

(kujazwa na mkopeseshaji wa kati baada ya idhini ya RFA) Tambua tarehe ya kukamilisha mkopo. Tuma nakala ya maombi ya mwisho ya mkopo kwa RFA.

BAADA YA KUTUMA MAOMBI

Baada ya kukamilisha ombi la mkopo na kupokea pesa, endelea kushirikiana kwa karibu na mkopeseshaji wa kati. Endelea kumwarifu mkopeseshaji wako kuhusu shughuli za kifedha zinazoathiri malipo ya mkopo huu. Mkopeseshaji wako wa kati pia atatumika kama rasilimali muhimu kwa maendeleo ya utendakazi wa shamba wenye mafanikio.